majira
GAZETI HURU LA KILA SIKU
www.timesmajira.co.tz
ISSN 0856-5086 ■ NA. 9118 • VOL. II/8219
Alhamisi 14 • MEI • 2020
BEI: TSHS 1000/KSHS 60

Vijana wawili wakutwa wamejinyonga Tunduru
Uk. 3

Papa amteua Askofu Nzigilwa kuongoza Jimbo la Mpanda
Uk. 4

Majaliwa: Nimeridhishwa ujenzi wa ofisi ya NEC
Uk. 3

Kiboye: CHADEMA wasipozingatia Warumi 13:1 chama kinasambaratika
Uk. 7

Wabunge Chadema marufuku Bungeni

●Kitengo cha Usalama cha Bunge chaagizwa kuwadhibiti kuanzia leo, wapo 15 wakiongozwa na Mbowe hadi watakapotimiza masharti Uk. 4

Serikali yatangaza bei elekezi ya chanjo 13

Na Mwandishi Wetu, Dodoma Dodoma

■■ SERIKALI imetangaza bei elekezi ya chanjo 13 za magonjwa ya mifugo ya kimkakati ambapo sasa wafugaji watapa ahueni kubwa kwa kutumia gharama ndogo kupata chanjo hizo huku Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina akitaka bodi ya Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania TVLA kuhakikisha Kliniki za mifugo zinajengwa kwenye halmashauri 185 kote nchini ifikapo Juni 2021 _Inaendelea Uk. 2

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina (kulia) akimkabidhi vitendea kazi Mwenyekiti mpya wa Bodi ya Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA), Profesa Amandus Muhairwa baada ya kuizindua bodi hiyo na kupokea taarifa ya kutangazwa kwa bei elekezi ya Chanjo Makao Makuu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mtumba jijini Dodoma. (Na Mpigapicha Maalum)

Polisi wamkamata Mdude kwa tuhuma za dawa za kulevya

Na Esther Macha, Mbeya

■■ JESHI la Polisi mkoani Mbeya linamshikilia, Mpaluka Mdude (32) mkazi wa Itezi Jijini Mbeya kwa tuhuma za kupatikana na unga unaodhaniwa kuwa ni dawa za kulevya aina ya Heroine gramu 23.4.

Mdude ambaye ni kada wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) alikuwa _Inaendelea Uk. 4

Mahakama yatoa hati ya kukamatwa Zitto UK. 4

Scanned with CamScanner

Serikali yakabidhi wavuvi injini za boti

Na Eleuteri Mangi, WHUSM, Dodoma

■■SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekabidhi injini nane za boti awamu ya pili kwa wabunge wa majimbo mbalimbali kwa lengo la kuvipatia vikundi vya ushirika vya uvuvi vilivyopo katika majimbo yao ili kusawaidia kuboresha utendaji kazi wao na kufanya shughuli za uvuvi wenye tija. Awali wizara hiyo ilitoa injini za boti tano na kufanya jumla ya injini zilizotolewa na wizara hiyo kufikia 13 ambazo thamani yake ni sh. milioni 60.

Akikabidhi injini hizo za boti juzi ijini Dodoma, Waziri wa Mifugo na Uvuvi Luhaga Mpina alisema Wizara yake inahimiza vyama vingine vya ushirika viboreshe utendaji wao wa kazi ili navyo viweze kupata ruzuku ya Serikali.

"Mtakubaliana na mimi kwamba wavuvi wetu wengi wanatumia zana duni sana na wanashindwa kufanya kazi zao za uvuvi kutokana na zana duni wanazotumia katika uvuvi na kutokana na zana zao hizo kuwa duni wanafanya kazi miaka nenda rudi lakini maisha yao hayabadiliki kutokana wanachopata ni kwa ajili ya chakula tu," alisema Waziri Mpina.

Ili kujua changamoto za wavuvi nchini, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imefanya tahmini kwa kuzunguka nchi nzima kujionea wananchi wanavyoendesha shughulizao za uvuvi ikiwemo changamoto wanazokutana nazo ambapo wamefanikiwa kuwaunganisha wavuvi katika vyama na vikundi mbalimbali ambavyo vinasaidia kurahisisha utendaji kazi ikiwemo kupata ruzuku kutoka Serikalini hatua inayowasaidia kufanya shughuli za uvuvi wenye tija kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Akitolea mfano wa vikundi vilivyonufaika na mikopo, Waziri Mpina alisema kuwa Wilaya ya Ukerewe imefanikiwa kuwa na vikundi vya wavuvi ambao wamenufaika na mikopo ya zaidi ya sh. milioni 500 na kufanya vyama vya ushirika nchini kufanikiwa kukopeshwa na taasisi za fedha zaidi ya sh. milioni 800.

Kwa upande wake Mbunge wa Kyela na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Dkt. Harrison Mwakyembe alisema kuwa wavuvi nchini wameanza kuchangamkia fursa zinazotolewa na Serikali ya Awamu ya Tano hatua ambayo itawafanya wawe na mafanikio makubwa kiuchumi.

Dkt. Mwakyembe alifafanua kuwa wilaya ya Kyelea ina mito mikubwa ya kudumu mine ikiwemo Kiwira, Songwe, Lufilio na Mbaka pamoja na ziwa Nyasa, lakini mazao ya samaki wilayani humo ni duni kutokana na mifaa duni vya uvuvi, hivyo injini ya boti aliyokabidhiwa itawasaidia wavuvi kuwa na uvuvi ambao utawasaidia kupata samaki wengi ambao watakidhi mahitaji ya soko.

Amesema injini hiyo itawasaidia wavuvi kuvua kiutaalamu zaidi na kwa usalama ikizingatiwa ziwa Nyasa kuna samaki wakubwa aina ya Mbasa ambao ni wakubwa kupita mitumbwi ya kawaida ambayo inatumiwa na wavuvi hao.

"Nina uhakika Wanakyela watahamasika kujiunga kwenye vikundi vya ushirika, wakulima hao hao wa Kyela ni sehemu ya wavuvi, wataunda vikundi imara, tutoke kwenye umasikini, tuongeze zaidi tija na mbinu za kisasa," alisema Dkt. Mwakyembe.

Aidha, Dkt. Mwakyembe amemthibitihia Waziri Mpina kuwa injini hiyo itawafikia wananchi na itatunzwa ili iweze kuwa na manufaa zaidi kwa wananchi wa Kyela.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Sekta ya Uvuvi Dkt. Rashid Tamatama amesema kuwa wavuvi wadogo wadogo wanachukua asilimia 85 ya wavuvi wote nchini ambapo samaki wote wanovuliwa ni karibu asilimia 90 wanavuliwa na wavuvi wadogo.

Katika mwaka 2019/2020, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imetambua vyama vya ushirika vya wavuvi vipatavyo 102 katika mikoa yote nchini hatua ambyo imesaidia pia kuhamasisha kuanzishwa vyama vipya 14 na kufanya jumla ya vyama vya ushirika vinavyotambuliwa na wizara hiyo kufuikia 116. Lengo la kuanzishwa vyama hivyo ni kuwawezesha wavuvi na wakuzaji viumbe maji kuwa na sauti ya pamoja ili waweze kupata mikopo na masoko ya bidhaa zao.

Vyama vya ushirika vilivyopata injini hizo za boti ni Magawa, Kisiju, Shungubweni vya mkoa wa Pwani, Mwamapuri wilaya ya Igunga mkoani Tabora, Mbamba Bay wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma, kikundi cha wavuvi Kyela mkoani Mbeya, kikundi cha Vita Fishing group Msanga Mkuu na Kikundi cha Jiwezeshe cha Nanyumbu mkoni Mtwara, Wakulima wa mwani Kwaigoma wilaya ya Handeni mkoani Tanga, Bukasige Finshing Cooperative Society cha Ukerewe mkoani Mwanza, kikundi cha wavuvi cha Nyamikoma cha Busega na kikundi cha wavuvi cha Kasanga Kalambo wanaofanya shaghuli zao eneo la ziwa Tanganyika.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina (wa pili kushoto), akimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Abel Yeji Busalama injini ya boti iliyotolewa na serikali kwa ajili ya kikundi cha wavuvi wilayani humo wakati wa makabidhiano yaliyofanyika juzi jijini Dodoma. (Picha Eleuteri Mangi, WHUSM, Dodoma)

Scanned with CamScanner

MAJIRA UK9

Bodi ya Nyama yafanya ziara kukagua kiwanda cha nyama

Na David John

KAIMU Msajili Bodi ya Nyama Tanzania, Iman Sichalwe amefanya ziara ya kuangalia maendeleo ya ujenzi wa kiwanda kikubwa cha nyama cha Tanchoice Soga kilichopo mjini Kibaha mkoani Pwani.

Kiwanda hicho ni kikubwa Afrika Mashariki na Kati kwenye sekta ya mifugo na kutajwa kuwa mkombozi mkubwa kwa wadau wa nyama nchini ambacho kitakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 1,000 na mbuzi 4,500 kwa siku.

Akiwa kiwandani hapo baada ya kufanya ukaguzi wa maendeleo ya ujenzi wa kiwanda hicho, Sichalwe alisema amejiridhisha kuwa kimekamilika kwa asilimia 99 na kilichobaki ni hatua za mwisho kuanza kufanya kazi na kuwataka Wafugaji kukaa mkao wa kula.

Pia alisema uwekezaji wa kiwanda hicho ni mkubwa kwenye sekta ya mifugo, ambao unatajwa kuleta matokeo chanya katika uchumi wa nchi.

Sichalwe aliwataka wafugaji kufuga kisasa na kuachana na kufuga kwa mazoea na kama bodi wenye dhamana kubwa ya kusimamia, kuendeleza na kuratibu sekta ya nyama nchini wataendelea kutoa elimu ya umuhimu wa uongezaji thamani ya mazao ya mifugo na kutambua namna bora ya kunenepesha mifugo, ili kupata nafasi ya kuuza mifugo yao kwenye kiwanda hicho.

Scanned with CamScanner

...siana na suala hilo,
...alisema kuwa yeye
...zungumzia chochote
...ke watafutwe wale
...amekuwa wakipewa

siwezi kulizungumzia suala hilo kwani muda bado, wakati ukifika nitasema kama nataka kugombea au hapana."

MAJIRA UK 11

...kikabidhi zawadi ya
...ra ya kuwapongeza
...u)

...a Mbeya

...eye changamoto nyingi
...mekuwa mnaifanya
...ama wawakilishi wa
...engine walioko kule
...naomba hizi salaam
...wao wauguzi ni jeshi
...unadhamini sana kazi
...wa ustawi wa hospitali
...a Dkt. Mbwanji.
...o Mkurugenzi huyo
...va katika huduma za
...auguzi ndio wanaokaa
...va kwa muda mrefu
...zima kukutana na
... nyingi na kutokana
...eendelea kuonesha
...do na ushirikiano kwa
...ukumu yao ya kufanya

Wafugaji wahimizwa kuzingatia kanuni

Na Oscar Mzuka, Dodoma

WAFUGAJI nchini wametakiwa kuzingatia kanuni za ufugaji bora kwa kuogesha mifugo yao, kuichanja na kuipatia dawa ya minyoo ili kuongeza tija katika ufugaji.

Hayo yalisemwa Jijini Dodoma jana na Msajili wa Baraza la Veterinari nchini, Dkt. Bedan Masuruli, alipokuwa akizungumza Majira kuhusu hatua zinazochukuliwa na Baraza hilo ili kuhakikisha vituo vyote vya Afya ya Wanyama nchini vinasajiliwa na vinakuwa na wataalam waliosajiliwa.

Dkt. Masuruli alisema viwango vilivyowekwa vya utoaji huduma na tiba ya wanyama inafanyika kwa kutumia dawa stahiki za wanyama na zilizosajiliwa nchini.

Aidha wafugaji wameaswa kuhakikisha wanapata huduma ya afya kwa mifugo yao kutoka Vituo vya Afya ya Wanyama vilivyosajiliwa na Baraza la Veterinari kwa kuwa vinao wataalam waliosajiliwa na wanazo sifa.

Alisema wataalam hao wamekidhi vigezo vyakutoa ushauri wa kitaalam kwa wafugaji na tiba kwa mifugo.

Vile vile wafugaji wametakiwa kuachana kuwatumia watu wasio na sifa za kuhudumia mifugo yao ambao wamekuwa wakiwasababishia hasara na kuwadangaya mambo ambayo yameendelea kudidimiza ufugaji.

Dkt. Masuruli alisema hivi sasa usimamizi wa dawa umeimarika kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na hatua kali zimeendelea kuchukuliwa kwa wale wanaokwenda kinyume na sheria.

Aliwataka wasambazaji wa dawa za mifugo nchini kuhakikisha dawa zimesajiliwa na zinakidhi viwango. Pia aliwasisitiza wafugaji kuzingatia hatua za kitaalam ili kulinda afya ya mifugo yao.

Scanned with CamScanner

ZIARA: Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (katikati) akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Idara ya Umeme wa Kiwanda cha Sukari Mtibwa, wakati alipofanya ziara ya kutembelea kiwanda hicho kufahamu hali ya upatikanaji wa umeme juzi.

MTANZANIA UK 17

Serikali yakabidhi wavuvi injini za boti za uvuvi

Na MWANDISHI WETU
-DODOMA

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekabidhi injini nane za boti awamu ya pili kwa wabunge wa majimbo mbalimbali kwa lengo la kuvipatia vikundi vya ushirika vya uvuvi kuvisaidia kuboresha utendaji kazi wao na kufanya shughuli za uvuvi wenye tija.

Awali wizara hiyo ilitoa injini za boti tano na kufanya jumla ya injini zilizotolewa na wizara hiyo kufikia 13 ambazo jumla zimegharimu Sh milioni 60.

Akikabidhi injini hizo juzi jijini Dodoma, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina alisema kuwa wizara yake inahimiza vyama vingine vya ushirika viboreshe utendaji wao wa kazi ili navyo viweze kupata ruzuku ya Serikali.

"Mtakubaliana na mimi kwamba wavuvi wetu wengi wanatumia zana duni sana na wanashindwa kufanya kazi zao za uvuvi kutokana na zana duni wanazotumia katika uvuvi.

"Kutokana na zana zao hizo kuwa duni wanafanya kazi miaka nenda rudi, lakini maisha yao hayabadiliki kutokana wanachopata ni kwa ajili ya chakula tu," alisema Mpina.

Akitolea mfano wa vikundi vilivyonufaika na mikopo, alisema kuwa Wilaya ya Ukerewe imefanikiwa kuwa na vikundi vya wavuvi ambao wamenufaika na mikopo ya zaidi ya Sh milioni 500 na kufanya vyama vya ushirika nchini kufanikiwa kukopeshwa na taasisi za fedha zaidi ya Sh milioni 800.

Kwa upande wake Mbunge wa Kyela na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe alisema kuwa wavuvi nchini wameanza kuchangamkia fursa zinazotolewa na Serikali ya Awamu ya Tano hatua ambayo itawafanya wawe na mafanikio makubwa kiuchumi.

Dk. Mwakyembe alifafanua kuwa Wilaya ya Kyela ina mito mikubwa ya kudumu minne ambayo ni Kiwira, Songwe, Lufilio na Mbaka pamoja na Ziwa Nyasa, lakini mazao ya samaki wilayani humo ni duni kutokana na vifaa duni vya uvuvi, hivyo injini ya boti aliyokabidhiwa itawasaidia wavuvi kupata samaki wengi ambao watakidhi mahitaji ya soko.

Alisema injini hiyo itawasaidia wavuvi kuvua kitaalamu zaidi na kwa usalama ikizingatiwa Ziwa Nyasa kuna samaki aina ya mbasa ambao ni wakubwa kupita mitumbwi ya kawaida ambayo inatumiwa na wavuvi hao.

"Nina uhakika Wanakyela watahamasika kujiunga kwenye vikundi vya ushirika, wakulima wa Kyela ni sehemu ya wavuvi, wataunda vikundi imara, tutoke kwenye umasikini, tuongeze zaidi tija na mbinu za kisasa," alisema Dk. Mwakyembe.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Sekta ya Uvuvi, Dk. Rashid Tamatama alisema kuwa wavuvi wadogo wadogo wanachukua asilimia 85 ya wavuvi wote nchini na kwamba samaki wote wanaovuliwa karibu asilimia 90 wanavuliwa na wavuvi wadogo.

Scanned with CamScanner

Hayo yameelezwa Dodoma jana na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, mdogo ya kilimo na biashara ambayo inawaingizia kipato kisichozidi Sh milioni nne, watanyabiashara wastaafu ambao kiwango chao cha mapato hakizidi kiasi hicho kwa mwaka.

– PICHA: MPIGAPICHA WETU

MSAADA: Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina (kushoto) akimkabidhi Mbunge wa Kyela ambaye pia ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe injini ya boti iliyotolewa na Serikali kwa kikundi cha wavuvi cha Kyela mkoani Mbeya wakati wa hafla ya makabidhiano ya injini hiyo Dodoma jana.

Costech, Taliri kuzalisha ng'ombe kwa teknolojia

Na MWANDISHI WETU
-DODOMA

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (Costech), imeiwezesha Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (Taliri) Mpwapwa kuzalisha ng'ombe kwa

Tathimini ya sekta ya mifugo inaonyesha kuwa ifikapo mwaka 2030 kutakuwa na upungufu wa nyama nyekundu kiasi cha tani 1,731,000 sawa na upungufu wa asilimia 33 ya mahitaji.

Mtafiti Mkuu wa Taliri Mpwapwa, ambaye pia ni mratibu

na kupandikizwa kwa ng'ombe jike waliopo kwenye joto.

"Teknolojia hii hujulikana kitaalamu kama uhaulishaji au 'artificial insemination'.

"Njia hii ni mbadala wa uzalishaji wa ng'ombe kwa njia ya asili inayotegemea ng'ombe jike mwenye joto kupandwa na ng'ombe dume

Hayo yamebainishw
na Mkurugenzi wa Asas
Wakulima wa Parachich
wa Njombe (Nshida), Fr
Msigwa.

Alisema kutokana
na changamoto hiyo,
imewalazimu kutafuta
Kampuni ya Ensol itaka
utafiti wa upatikanaji w
katika mashamba ya w
wa parachichi.

"Sasa hivi uhitaji wa
parachichi umekuwa ni
mkubwa sana duniani a
uzalishaji wetu umekuw
mdogo, sababu kubwa
tumeiona inayopelekea
wazalishaji kuwa mdog
maji, parachichi zinahit
maji, hasa wakati wa k

"Tumeamua kualik
Kampuni ya Ensol amb
wanajishughulisha na
wa jua, wamekuja kufa
utafiti kwenye mashan
wakulima ili tuweze ku
tutawasaidia vipi waku
waweze kupata maji il
waongeze uzalishaji,"
Msigwa.

Kwa upande wake,
Meneja mradi wa Kam
Ensol, Lameck Kanshe
alisema wamefika mk
Njombe kufanya utafit
mashamba ya wakulim
parachichi ili kuwasaid
kuweza kupata maji.

"Wakulima wanat
nguvu nyingi katika
kumwagilia kwa saba
parachichi zinahitaji
muda wote, sasa una
mkulima ana heka nn
tano, huwezi kuzihud
kuchota maji.

"Mkulima anawe
kuwa anachota maji
baiskeli, pikipiki na v
mwengine kwa kuko
kwenda kuchota ma
kumwagilia masham

"Kwa hiyo kwanz
wanatumia gharama
na nguvu kubwa kuh
ekari chache walizo
lakini kama watapat
ya kumwagilia wana
kuhudumia mashan
makubwa hekari ku
kwa urahisi zaidi,"
Kanshenshe.

Kwa upande wa

Scanned with CamScanner

ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe injini ya boti iliyotolewa na Serikali kwa kikundi cha wavuvi cha Kyela mkoani Mbeya wakati wa hafla ya makabidhiano ya injini hiyo Dodoma jana.

MTANZANIA UK 18

Costech, Taliri kuzalisha ng'ombe kwa teknolojia

Na MWANDISHI WETU
-DODOMA

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (Costech), imeiwezesha Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (Taliri) Mpwapwa kuzalisha ng'ombe kwa kutumia teknolojia ya urutubishaji na upandikizaji wa viinitete.

Taarifa za Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) zinaonyesha kuwa Tanzania ni nchi ya tatu barani Afrika kwa wingi wa mifugo, hasa ng'ombe ikifuatiwa na nchi za Ethiopia na Sudan (kabla haijagawanyika).

Hata hivyo asilimia 98 ya ng'ombe wanaofugwa Tanzania ni wa kienyeji ambao hawana nyama nyingi na hawazalishi maziwa kwa wingi.

Tathimini ya sekta ya mifugo inaonyesha kuwa ifikapo mwaka 2030 kutakuwa na upungufu wa nyama nyekundu kiasi cha tani 1,731,000 sawa na upungufu wa asilimia 33 ya mahitaji.

Mtafiti Mkuu wa Taliri Mpwapwa, ambaye pia ni mratibu mkuu wa mradi huo, Dk. Kabuni Thomas, alisema kwa kulitambua hilo, Costech kwa kushirikiana na Taliri Mpwapwa inatekeleza mradi wa kuzalisha ng'ombe wenye tija kwa lengo la kusaidia upatikanaji wa malighafi zitokanazo na mazao ya mifugo; mfano, maziwa, nyama na ngozi.

Alisema katika kila mshindo mmoja wa fahari dume hupatikana zaidi ya mbegu 500 ambazo huvunwa na kupandikizwa kwa ng'ombe jike waliopo kwenye joto.

"Teknolojia hii hujulikana kitaalamu kama uhaulishaji au 'artificial insemination'.

"Njia hii ni mbadala wa uzalishaji wa ng'ombe kwa njia ya asili inayotegemea ng'ombe jike mwenye joto kupandwa na ng'ombe dume ambaye hutumia mbegu zaidi ya 500 katika kuzalisha ndama mmoja.

"Kitaalamu mbegu moja tu kutoka kwenye ng'ombe dume huhitajika kuzalisha ndama mmoja.

"Hivyo kuzalisha ng'ombe kwa njia ya asili husababisha upotevu mkubwa wa mbegu kutoka kwa ng'ombe dume zinazotumika katika kuzalisha ndama mmoja," alisema Dk. Kabuni.

Scanned with CamScanner

Barua pepe: tanzaniadaima@gmail.com

Kitaifa

MSAADA

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina (wa pili kushoto), akimkabidhi injini ya boti, Mbunge wa Mtwara Vijijini, Hawa Ghasia (kulia), kwa ajili ya kusaidia vikundi vya ushirika wa wavuvi Mtwara Vijijini. Injini hiyo ni sehemu ya injini 13 zenye thamani ya Sh. Milioni 60 zilizotolewa bure na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya kusaidia wavuvi katika maziwa, mito, mabwawa na bahari. (Picha na Wizara ya Mifugo)

Scanned with CamScanner

Wanafunzi wenye mahitaji maalumu wa Shule ya Msingi ya Kalesh 'A', wilayani Hanang' wakiingia kwenye bwalo maalumu la kulia chakula lililojengwa hivi karibuni na kuondokana na adha waliyokuwanayo ya kula chini ya miti. (Picha na Jumbe Ismailly)

TANZANIA DAIMA

Chanjo 13 zapangiwa bei elekezi

NA MWANDISHI WETU, DODOMA

SERIKALI imetangaza bei elekezi ya chanjo 13 za magonjwa ya mifugo ya kimkakati ambapo sasa wafugaji watapata ahueni kubwa kwa kutumia gharama ndogo kupata chanjo hizo.

Pia, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina aliitaka Bodi ya Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) kuhakikisha Kliniki za mifugo zinajengwa kwenye halmashauri 185 kote nchini ifikapo Juni, mwaka 2021.

Akitangaza bei elekezi wakati wa uzinduzi wa Bodi ya Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) Dodoma, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Tanzania, Profesa Hezron Nonga alisema, bei hiyo itaanza kutumika leo na kwamba wafugaji na wafanyabiashara wote wanapaswa kufuata bei hiyo iliyotangazwa na Serikali.

Prof. Nonga alizitaja bei elekezi hizo kuwa ni pamoja ya Chanjo ya Homa ya Mapafu ya Ngombe (CBPP) bei ya dukani kwa dozi itauzwa Sh. 300 huku bei ya uchanjaji kwa mfugo ikiwa ni Sh. 550, Chambavu (Black quarter) dozi dukani Sh. 500 kwa mfugo atachanjiwa Sh. 800.

Profesa Nonga alisema Kimeta (Anthrax) dozi dukani ni 250 na kwa mfugo itakuwa Sh. 500, Mchanganyiko wa Chambavu na Kimeta (TECOBLAX) kwa Ng'ombe dozi dukani Sh. 560 na kwa mfugo utachanjwa kwa Sh. 800, Mchanganyiko wa Chambavu na Kimeta (TECOBLAX) kwa mbuzi na kondoo dozi dukani Sh. 280 kwa mfugo ni Sh. 500.

Pia ugonjwa wa Kutupa Mimba (Brucellosis) dozi dukani ni 1,000 na kwa mfugo ni Sh.1,500, Mdondo (Newcastle disease) dozi ni Sh.50 na mfugo ni Sh.50, Mapele Ngozi (Lumpy Skin Disease) kwa ng'ombe dozi dukani ni Sh. 400 na kwa mfugo ni Sh. 600 huku Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR) dozi dukani ni Sh. 200 na kwa mfugo ni Sh.350. Pia Homa ya mapafu ya mbuzi (CCPP) dozi dukani ni 200 na mfugo itakuwa ni Sh.350, Ugonjwa wa Miguu na Midomo (FMD) dozi dukani ni Sh. 2,500 na kwa mfugo ni Sh.3,000, Kichaa cha Mbwa (Rabies) dozi dukani ni Sh.1,000 kwa mfugaji ni Sh. 1,500.

Profesa Nonga aliongeza kuwa ugonjwa wa Ndigana Kali (ECF) dozi dukani ni Sh. 10,000 na kwa mfugo ni Sh. 17,000 huku Homa ya Bonde la Ufa (RVF) dozi dukani ni Sh. 400 huku kwa mfugo ikiwa ni Sh. 700.

Akizungumza mara baada ya kuzindua Bodi hiyo ya TVLA, Mpina alisema kupitia mabadiliko hayo ya Kanuni za kutoa bei elekezi, Serikali itakuwa imepunguza gharama kwa wafugaji kutoka Sh. Bilioni 482.4 walizokuwa wakizitumia kununua chanjo hadi kufikia Sh. Bilioni 237 ikiwa ni punguzo la asilimia 51.

Mpina aliitaka bodi hiyo mpya kufanya kazi usiku na mchana kuwalea wafugaji wa Tanzania kupitia eneo hilo muhimu la chanjo na matibabu ya mifugo na kuchochea ongezeko la uzalishaji mifugo hali itasaidia kuhudumia viwanda vya mazao ya mifugo vinavyojenga maeneo mbalimbali nchini.

Pia aliitaka bodi hiyo kukomesha matumizi ya dawa feki na zilizomaliza muda wake, kurahisisha upatikanaji wa chanjo hatua itakayowezesha kuendelea kupungua kwa magonjwa na kuweza kuongeza masoko na ushindani kimataifa.

Waziri huyo aliiagiza bodi hiyo kuhakikisha kuwa ifikapo Juni, mwaka 2021 chanjo 7 ambazo ziko katika hatua mbalimbali zizalishwe hapa nchini ili kuwawezesha wafugaji kuzipata kwa urahisi na kwa gharama nafuu.

Pia Waziri Mpina aliitaka bodi kuhakikisha kuwa ujenzi wa kliniki za mifugo kwa halmashauri zote 185 kote nchini pamoja na mikoa 15 ambayo haina maabara kwa sasa ziwe zimekamilika ifikapo Juni, mwaka 2021.

Mwenyekiti wa Bodi ya TVLA, Profesa Amandus Muhairwa alimhakikisha Waziri Mpina kuwa watatumia weledi wao wote kuhakikisha wanatekeleza maagizo yote aliyoyatoa ili kuiwezesha Sekta ya Mifugo kupita hatua kubwa kwa kipindi chote cha uongozi wao.

Scanned with CamScanner

TAHARIRI / KIBON

uk 9

TanzaniaDaima

Wafugaji waitumie vizuri nafuu bei ya chanjo

MOJA ya habari katika vyombo vya habari leo, ni Serikali kutangaza bei elekezi ya chanjo 13 za magonjwa ya mifugo ya kimkakati ambapo sasa wafugaji watapa ahueni kubwa kwa kutumia gharama ndogo kupata chanjo hizo.

Pia, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina aliitaka bodi ya Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania TVLA kuhakikisha Kliniki za mifugo zinajengwa kwenye halmashauri 185 kote nchini ifikapo Juni, mwaka 2021.

Akitangaza bei elekezi wakati wa uzinduzi wa Bodi ya Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) Dodoma, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Tanzania, Prof. Hezron Nonga alisema bei hiyo itaanza kutumika leo.

Kwamba, chini ya nafuu hiyo wafugaji na wafanyabiashara wote wanapaswa kufuata bei hiyo iliyotangazwa na Serikali.

Prof. Nonga alizitaja bei elekezi hizo, ni pamoja ya Chanjo ya Homa ya Mapafu ya Ngombe (CBPP) bei ya dukani kwa dozi itauzwa Sh. 300 huku bei ya uchanjaji kwa mfugo ikiwa ni Sh. 550, Chambavu (Black quarter) dozi dukani Sh. 500 kwa mfugo atachanjiwa Sh. 800.

Alisema, Kimeta (Anthrax) dozi dukani ni 250 na kwa mfugo itakuwa Sh. 500, Mchanganyiko wa Chambavu na Kimeta (TECOBLAX) kwa Ng'ombe dozi dukani Sh. 560 na kwa mfugo utachanjwa kwa Sh. 800.

Aidha, mchanganyiko wa Chambavu na Kimeta (TECOBLAX) kwa mbuzi na kondoo dozi ni kwa Sh. 280 kwa mfugo ni Sh. 500.

Pia ugonjwa wa Kutupa Mimba (Brucellosis), dozi dukani ni 1,000 na kwa mfugo ni Sh.1,500, Mdondo, dozi ni Sh.50 na mfugo ni Sh.50, Mapele Ngozi kwa ng'ombe dozi dukani ni Sh. 400 na kwa mfugo ni Sh. 600 huku Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR) dozi dukani ni Sh. 200 na kwa mfugo ni Sh.350.

Aidha, Homa ya mapafu ya mbuzi (CCPP) dozi dukani ni 200 na mfugo itakuwa ni Sh.350, Ugonjwa wa Miguu na Midomo (FMD) dozi dukani ni Sh. 2,500 na kwa mfugo ni Sh.3,000, Kichaa cha Mbwa dozi dukani ni Sh.1,000 kwa mfugaji ni Sh. 1,500.

Profesa Nonga aliongeza kuwa ugonjwa wa Ndigana Kali (ECF) dozi dukani ni Sh. 10,000 na kwa mfugo ni Sh. 17,000 huku Homa ya Bonde la Ufa (RVF) dozi dukani ni Sh. 400 huku kwa mfugo ikiwa ni Sh. 700.

Akizungumza mara baada ya kuzindua Bodi hiyo ya TVLA, Mpina alisema kupitia mabadiliko hayo ya Kanuni za kutoa bei elekezi, Serikali itakuwa imepunguza gharama kwa wafugaji kutoka Sh. Bilioni 482.4 walizokuwa wakizitumia kununua chanjo hadi kufikia Sh.Bilioni 237 ikiwa ni punguzo la asilimia 51.

Mpina aliitaka bodi hiyo mpya kufanya kazi usiku na mchana kuwalea wafugaji wa Tanzania kupitia eneo hilo muhimu la chanjo na matibabu ya mifugo na kukuchochea ongezeko la uzalishaji mifugo hali itasaidia kuhudumia viwanda vya mazao ya mifugo vinavyojengwa nchini.

Pia, aliitaka bodi hiyo kukomesha matumizi ya dawa feki na zilizomaliza muda wake, kurahisisha upatikanaji wa chanjo hatua itakayowezesha kuendelea kupungua kwa magonjwa na kuweza kuongeza masoko na ushindani kimataifa.

Waziri huyo aliiagiza bodi hiyo kuhakikisha kuwa ifikapo Juni, mwaka 2021 chanjo 7 ambazo ziko katika hatua mbalimbali zizalishwe hapa nchini ili kuwawezesha wafugaji kuzipata kwa urahisi na kwa gharama nafuu.

Pia, Waziri Mpina aliitaka bodi kuhakikisha kuwa ujenzi wa Kliniki za mifugo kwa halmashauri zote 185 kote nchini pamoja na mikoa 15 ambayo haina maabara kwa sasa ziwe zimekamilika ifikapo Juni, mwaka 2021.

Mwenyekiti wa Bodi ya TVLA, Prof. Amandus Muhairwa alimhakikisha Waziri Mpina kuwa watatumia weledi wao kuhakikisha wanatekeleza maagizo yote aliyoyatoa ili kuiwezesha Sekta ya Mifugo kupita hatua kubwa kwa kipindi chote cha uongozi wao.

Sisi Tanzania Daima, tunapongeza hatua ya serikali kupunguza gharama za dawa za mifugo ambazo kwa muda mrefu ulikuwa ni mzigo mkubwa hasa kwa wafungaji wenye mifugo mingi.

Tunaamini, hii ni ahueni kubwa kwa wafugaji katika maeneo mbalimbali nchini katika kipindi hiki cha nchi kuelekea katika Uchumi wa Kati hapo itakapofika 2025 huku viwanda ikiwa kama injini ya kufikia lengo hilo.

Mtaa wa Kondoa/Fundikira, Magomeni
SLP 15261, Dar es Salaam. Simu: 2126232 Fax: 2126234
Chumba cha Habari
Barua pepe: daimahabari@gmail.com, daimanews@yahoo.com
Simu: +255 768 477 277, +255 716 730 912, +255 718 975 731
Tovuti: www.freemedia.co.tz

Kaimu Mhariri Mtendaji:	Martin Malera	+255 713 260 071
Mhariri wa Habari	Arodia Peter	+255 717 4142 78
Mhariri wa Makala	Suleiman Msuya	+255 716845187
Mhariri wa Michezo	Tulio Chambo	+255 752462103
Msambazaji Mkuu	Shukuru Kapaka	+255 718795328

Corona

MTAZAMO

NA SULEIM

msuyasule@gma

COVID-19 osababishwa n ambao kihist katika jimbo China, Desemb

Kwa mujib Afya Duniani COVID-19 ime zote duniani n ya watu milio huku vifo viki na waliopona milioni 1.5.

Kimsingi miezi mitano ruga mifumo na mingine zote duniani ikiwa ndio in biliana na ha

Ni kupitia usafiri wa umefungwa, kwa ujumla kwa baadhi na watu.

Kutokana shughudia zikifanywa iani ikiwem kwa maji kutumia v taiza', Bara mikusanyik kufungwa ikiwemo ib

Jitihada fulani zina majibu n shaka kuv yamekuw

Scanned with CamScanner

ELIMU & UFAHAMU

MANGI HOROMBO: KIONGOZI WA WACHAGA MWENYE MAAJABU

UK 10

COSTECH ilivyoiwezesha TALIRI kuzalisha ng'ombe kwa Viini tete

NA MWANDISHI WETU

TAARIFA za Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) zinaonyesha kuwa Tanzania ni Nchi ya tatu barani Afrika kwa wingi wa mifugo hasa ng'ombe ikifuatia na nchi za Ethiopia na Sudan (kabla haijagawanyika Sudani Kusini na Sudan).

Hata hivyo asilimia 98 ya ng'ombe wanaofungwa Tanzania ni wa kienyeji ambao hawana nyama nyingi na hawazalishi maziwa kwa wingi.

Tathimini ya sekta ya mifugo inaonyesha kuwa ifikapo mwaka 2030 kutakuwa na upungufu wa nyama nyekundu kiasi cha tani 1,731,000 sawa na upungufu wa asilimia 33 ya mahitaji.

Upungufu huo utachangiwa zaidi na changamoto za ubora hafifu wa mifugo, hasa ng'ombe wanaofungwa Tanzania ikiwa pamoja na makadirio ya kuwepo na ongezeko kubwa la idadi ya watu hasa watakao hamia mijini ifikapo mwaka 2030.

Hizo ni baadhi ya changamoto zinazokabili sekta ya mifugo nchini na ni wajibu wa kila mdau wa maendeleo kufikiri namna bora ya kutatua changamoto hizo.

Kutokana na hali hiyo Serikali inahamasisha uchumi wa viwanda unaolenga kwenye ujenzi wa viwanda vitakavyo tumia malighafi za ndani.

Mtafiti Kiongozi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) iliyopo wilayani Mpwapwa Mkoa wa Dodoma Dk.Kabuni Thomas Kabuni akionesha waandishi wa habari (hawapo pichani) namna wanavyovuna mbegu kutoka kwa ng'ombe dume kabla ya kuzipandikiza kwa ng'ombe jike(Picha na mpigapisha wetu)

Viwanda hivyo vinahitaji uwepo endelevu wa malighafi kwa ajili ya kuzalisha bidhaa mbalimbali.

Kutokana na changamoto zilizojitokeza kuna umuhimu mkubwa wa kuboresha sekta ya mifugo ili kufanikisha upatikanaji endelevu wa malighafi za mifugo na kusaidia nchi kufikia azma yake ya kuwa na uchumi wa kati unao ongozwa na sekta ya viwanda.

Kwa kulitambua hilo, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) iliyopo wilayani Mpwapwa Mkoa wa Dodoma inatekeleza mradi wa kuzalisha ng'ombe wenye tija kwa lengo la kusaidia upatikanaji wa malighafi zitokanazo na mazao ya mifugo kama, maziwa, nyama na ngozi.

Katika kuhakikisha kuwa kuna ng'ombe wa kisasa na wa kutosha, TALIRI kupitia mradi unaofadhiliwa na COSTECH imetafuta njia bora ya uzalishaji wa ng'ombe wenye tija.

Njia hiyo inatumia teknolojia ya uvunaji wa mbegu za fahari kutoka kwa ng'ombe dume. Katika kila mshindo mmoja wa

INAENDELEA UK.12

Scanned with CamScanner

NIPASHE UK 15

Wafugaji waiangukia serikali utatuzi kero

Na Augusta Njoji, DODOMA

SERIKALI imeombwa kutatua kero zinazowakabili wafugaji nchini kutokana na kutokuwa na mfumo mzuri wa uwasilishaji wa kero hizo.

Kadhalika, wafugaji hao wamesema kwa sasa hawana uongozi wa kitaifa unaotambulika kisheria ukaowasilisha kero zao kwenye mamlaka sahihi ili kushughulikiwa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana, mmoja wa wafugaji kutoka Wilaya ya Manyoni, Ally Someko, alisema miongoni mwa kero hizo ni kutozwa bei tofauti ya chanjo.

Alisema wanasikitishwa bei elekezi ya chanjo ni Sh 250 hadi 300, lakini chanjo iliyofanyika miezi iliyopita walilazimika kulipa Sh. 1,000 kwa ng'ombe.

Aliomba serikali kusaidia kushughulikia kero zinazolalamikiwa na wafugaji ili wawe na ufugaji wenye tija na kupatikana kwa maeneo ya kufanya shughuli zao.

"Wafugaji wana kero nyingi, lakini hatuna viongozi wa kuziwasilisha tuna kamati ya mpito ambayo viongozi wake walitakiwa kukoma tangu mwaka 2017 lakini wapo kwa maslahi yao na si kuwasemea wafugaji," alisema.

Naye Mathew Masele alisema Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), kwa sasa hakuna mazingira rafiki ya kushughulikia migogoro ya kati ya wafugaji na wakulima, na kutaka kuwapo mfumo mzuri wa kuwasilisha serikalini ili kutafutiwa ufumbuzi.

Desemba mwaka 2018, mkutano wa uchaguzi wa chama hicho ulivunjika, baada ya kubainika dosari mbalimbali ikiwamo kuwapo na wajumbe mamluki na migogoro ya kiuongozi, hivyo hadi sasa hakuna uchaguzi uliofanyika.

"Wafugaji wana kero nyingi, lakini hatuna viongozi wa kuziwasilisha tuna kamati ya mpito ambayo viongozi wake walitakiwa kukoma tangu mwaka 2017 lakini wapo kwa maslahi yao na si kuwasemea wafugaji," alisema.

Chi
ku
Na Augu
WIZARA
unda timu
sekta mb
irika nchi
kuboresh
Pia, im
kwa ajili
tikana kw
kutoathir
Ushar
na Mbur
dallah C
hotuba
mwaka 2
Alise
kezo ya
wa msa
wakulim
"Ush
bilio la
changar
uliza ch
ya mwa
na je, t
Ushirik

Nail
kuk
Kus
Na
Ka
ta
m
w
al
k
n
b
c
r

Scanned with CamScanner

there are others who took loans from the situation among Tanzanian farmers. had seized to purchase their product

THE GUARDIAN Page no. 5.

Livestock and Fisheries minister Luhaga Mpina (2nd-L) presents to Kaliua (Tabora Region) district commissioner Abel Yeji Busalama a speed boat engine the government has donated to a group of fishermen based in the district. This was at a ceremony held in Dodoma city. Photo: Guardian Correspondent

Three sea operation

By Guardian Reporter, Zanzibar

ZANZIBAR Minister of State (Regional Administration and Local Government) Haji Omar Kheir has said three centres for rescue at sea that will assist in rescue work from various disasters at sea have already been completed.

Tabling his budget estimates for his Office for Financial year 2020/21, he mentioned the rescue centres as the one at Kibweni in Zanzibar Urban West Region, Nungwi in Zanzibar North Region and Mkoani in Pemba.

He said these centres have been installed with communication equipment on disasters when they happen.

Kheir said the equipment is able to identify and locate the positions of vessels in distress to enable rescue operations to take place.

He initia Presi Shein accid passe He

Scanned with CamScanner